

**TV za London zinageuzwa
kuwa na mfumo wa kidijiti
kuanzia April 2012**



Kitu gani kinaendelea?

Mfumo wa zamani wa kurusha matangazo ya TV utazimwa na kuanzia mwezi **April 2012** kutakuwa na mfumo mpya utakaotumia ishara mfumo wa dijiti ambao ni wa kasi na nguvu zaidi.

1

Natakiwa nifanye nini?

Kama una:

- **Freeview, BT Vision au Top Up TV:**
Itabidi urekebishe TV yako au kisanduku cha kigeuzi cha TV kuanzia mwezi April. Tazama **ukurasa wa 4** ujue namna ya kurekebisha
- **Sky TV, Virgin au Freesat:**
Kama unapata mojawapo ya huduma hizi katika TV zako ZOTE huna haja ya kufanya chochote
- **TV isiyo ya kidijiti** (inayonasa idhaa tano tu):
Badilisha TV yako iwe na kinasaji cha kidijiti la sivyo hautaweza kupokea utangazaji wa ishara za kidijiti kutoka kwa idhaa za televisheni baada ya mwezi April 2012.

2

Mabadiliko haya yataanza lini?

Kuanzia mwezi **April 2012** mfumo wa zamani wa kutangaza katika TV utazimwa na kubadilishwa na kutakuwa na mfumo mpya unaotumia ishara za kidijiti. Utaratibu huu utafanywa kwa hatua mbili:

Tarehe 4 April

BBC Two itazimwa

Tarehe 18 April

**BBC One, ITV, Channel 4 na
Channel 5 zitazimwa**

Idhaa hizi zitabadilishwa na kutakuwa na vipindi vya kidijiti.

3 Je, mashine ya video bado itaweza kufanya kazi?

Baada ya mwezi April 2012, kama mashine ya video au DVD yako haitakuwa katika mfumo wa Dijiti haitaweza kurekodi kipindi chochote wakati unapoangalia kipindi kingine. Ni TV inayonasa mfumo wa *kidijiti* ndio itakayoweza kufanya hivyo.

4 Naweza kupataje TV ya kidijiti?

Unaweza kuchagua huduma yoyote kama vile Freeview, au tafuta huduma inayotumia setilaiti au nyaya kama vile Sky TV au Virgin, au nunua TV yenye mfumo wa kidijiti. Baadhi ya huduma kadhaa, kama vile Freeview na Freesat zinapatikana kwa malipo yanayofanywa mara moja. Huduma zingine kama vile Sky TV, zinahitaji malipo ya kila mwezi.

5 Ni wakati gani ninaweza kurekebisha TV yangu?

Kama una Freeview, itabidi urekebisha TV yako kuanzia tarehe **4 April** na tarehe **18 April**. Pia, itabidi urekebisha kama kutakuwa na vipindi vya TV ambavyo havionekani.

6 Ninarekebishaje TV yangu?

Unarekebisha ukitumia remote control yako. Unafanya ifuatavyo:

- 1 Washa Freeview TV yako au kisanduku. Halafu bonyeza **'menu'** katika remote control yako.
- 2 Chagua **'set up'** au **'installation'**. Au kama unaona picha katika remote control yako, chagua picha ya kisanduku cha vifaa, dishi la setilaiti au picha yenye spana.
- 3 Kama ukiombwa uweke tarakimu, bonyeza **0000** au **1234**
- 4 Chagua **'full re-tune'**. Hii wakati mwingine inaitwa **'first time installation'**, **'factory reset'**, **'default settings'** au **'shipping conditions'**.
Usichague **'channel update'** au **'add channels'**.
- 5 Bonyeza **'OK'** kama ukiambiwa futa vipindi vyote.
- 6 Vipindi vyote vitajiweka vyenyewe. TV yako inaweza ikazimika na kujiwasha upya.



7 Kuhusu kinasawimbi cha nje (aerial) cha TV yangu?

Utahitaji tu kinasawimbi cha nje kama utatumia Freeview, BT Vision au Top Up TV. Kama ukipata picha nzuri, inawezekana usihitaji kununua kinasawimbi kipya.

8 Endapo ninaishi kwenye magorofa?

Kama unaishi kwenye magorofa, inawezakana televisheni yako inapokea ishara kwa kutumia kinasawimbi cha nje cha jengo nzima. Utahitaji kuongea na msimamzi wa jengo lako ili kujua kama mnapokea ishara ya kidijiti.



9 Kuna msaada zaidi?

Kama una miaka 75 au zaidi, au una ulemavu wa aina fulani, unaweza kupata msaada kutoka Help Scheme, ambayo inaendeshwa na BBC.

Utapata:

- Vifaa ambavyo ni rahisi kutumia
- Fundi atakayekuja na vifaa na atakuunganishia vifaa hivyo
- Huduma ya miezi kumi na mbili ya maangalizi na kukusaidia kurekebisha

Gharama ya huduma hii ni paundi **£40** lakini inatolewa bure kama unapokea ruzuka ya aina fulani. Ofisi ya Help Scheme itakuandikia lakini unaweza kuwapigia ukitumia simu ya bure ambayo namba yake ni **0800 40 85 900** na omba utafutiwe mtafsiri.




BBC

Help Scheme inaendeshwa na BBC

 **switchover**
help scheme

10 Naweza kupata wapi maelezo zaidi?



Unaweza kupiga nambari hii ya simu **08456 50 50 50*** ili uonge na mshauri kwa lugha ya Kiingereza, au unaweza kuwambia wakutafutie mtafsiri.

Na pia, unaweza kupata mawasiliano zaidi ukitazama tovuti yetu iliyoandikwa kwa Kiingereza **digitaluk.co.uk**



get set for digital

*Wateja wa BT wanaweza kupiga simu bure. Wateja wa kampuni zingine watalipa gharama ambazo zinatofautiana. Saa za kawaida za kazi za Digital UK ni saa 2 asubuhi hadi saa 1 jioni (8am to 7pm) Jumatatu hadi Ijumaa, na Jumamosi ni saa 3 asubuhi hadi saa 11 jioni (9am to 5pm). Jumapili ofisi inafungwa. Wakati wa kipindi cha mageuzi saa za kazi zitaongezwa katika kila eneo. Digital UK, PO BOX 26833, Kirkcaldy, KY2 9AG